## 3.0 USAJILI WA TALAKA

### 3.1 Ni upi uthibitisho wa talaka?

Uthibitisho wa talaka ni ithibati (tarjis ya talaka) kutoka kwa wathibitishaji talaka kama vile, Kadhi (Sheikhe) Padri au Mkuu wa Mkoa.

### 3.2 Kuna aina ngapi za usajili wa talaka?

Kuna aina mbili za usajili wa talaka ambazo ni usajili wa talaka ndani ya wakati (ndani ya siku 30) na usajili wa talaka nje ya wakati (baada ya kupita siku 30 tangu kuvunjika kwa ndoa)

### 3.3 Ni upi utaratibu wa kusajili talaka?

Zipo aina mbili za taratibu za usajili wa talaka ambazo ni: -

- **Ndani ya wakati**

Utaratibu za kusajili talaka ndani ya wakati (siku 30 baada ya talaka kutolewa) ni kama ifuatavyo:

i. Kuwasilisha uthibitisho wa tukio la talaka (tarjis ya talaka) kutoka kwa wathibitishaji talaka;
ii. Kuwasilisha nakala ya cheti cha ndoa iliyovunjika;
iii. Kuwasilisha nakala ya kitambulisho cha muombaji kinachotambulika na serikali; na
iv. Kuwasilisha uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (kanuni ya 19(a) ya kanuni za wakala wa usajili wa matukio ya kijamii zanzibar 2020)

- **Nje wa wakati**

Utaratibu wa usajili wa talaka nje ya wakati (baada ya siku 30 kutolewa talaka) ni kama ifuatavyo:

i. Kuwasilisha uthibitisho wa talaka kutoka Mahkama ya Kadhi au Amri ya talaka ya Mahkamani;
ii. Kuwasilisha Nakala ya cheti cha ndoa iliyovunjika;
iii. Kuwasilisha Nakala ya kitambulisho cha muombaji kinachotambuka na Serikali; na
iv. Uthibitisho mwengine wowote utakaohitajika. (Kanuni ya 19(b) ya Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 2020)

### 3.4 Ni zipi athari za kutokusajili talaka?

kutokusajili talaka na kutokuwa na cheti cha talaka ni kosa kwa mujibu wa sheria, kosa ambalo linapelekea athari zifuatazo: -

